JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 26 - 2019/2020**

**DHIDI YA**

**CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO**

**UAMUZI**

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA UTANGAZAJI WA REDIO NA TELEVISHENI), 2018.**

## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilitoa leseni ya kurusha Matangazo (Matangazo ya Redio) kwa kituo cha **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** kwa ajili ya kutoa huduma ya utangazaji wa maudhui kwa njia ya Redio.

1.2 Tarehe 04 Juni, 2020 kati ya Saa 10.00 na Saa 12.00 jioni, **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** kupitia kipindi cha **Jahazi** wanatuhumiwa kukiuka Sheria, Kanuni na Maadili ya Utangazaji kwa kurusha maudhui yenye kuhamasisha ufanyaji wa vitendo vya ngono na utumiaji wa supu ya pweza katika kuimarisha tendo la ndoa katika muda ambao wasikilizaji wanaweza kuwa watoto.

1.3 Watangazaji wa kipindi cha **Jahazi** walisikika wakishabikia jinsi ambavyo watu wanavyoweza kupata hamu zaidi ya kufanya mapenzi baada ya kutumia mchuzi wa pweza na kwamba katika kuutumia mchuzi huo unaleta hamasa na kutoa nguvu zaidi kwenye tendo la ndoa. Walisema hiyo siyo siri tena kwa sababu ya uthibitisho wa kisayansi kutoka katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili.

1.4 Maudhui ya kipindi hayakuzingatia suala la kumlinda mtoto asiweze kuathiriwa na maudhui yasiyofaa na yenye vionjo vya ngono kwa kuwa kipindi hicho kimetangazwa muda ambao watoto wengi ni sehemu ya wasikilizaji wa redio. Watangazaji hawakupaswa kutangaza maudhui ya watu wazima yenye kuhamasisha ufanyaji wa tendo la ndoa na ngono kwani inaweza kuchochea vijana na watoto kutaka kujaribu na kuwafanya kuiga tabia mbaya. Yafuatayo ni baadhi ya maneno ambayo yametolewa na watangazaji wa kipindi husika:

***"...Mtangazaji 1: "Umeona eeh mara nyingi lishaulizwa sana hili swali nakumbuka sijui ni dokta Aizaki au mtu mwingine aliwahi kutoa ufumbuzi wa kuna aina gani ya kirutubishi ndani ya mchuzi wa pweza naaa kikiingia kwenye mwili wa binadamu kile kirutubisho ni ukweli kinakwenda kusisimua mwili na mtu anapata"***

***Mchangiaji: ("sexual desire") ...anapata hamu zaidi ya kufanya mapenzi...anapata nguvu zaidi ya kwenye tendo la ndoa.***

***Mtangazaji 2 (Dj Fetty): "Eh na kwa habari ambayo ...pale MUHAS Muhimbili pale walisema it's not a myth anymore lakini ni scientifically proven ...lakini wamezungumzia zaidi kwa wanaume...mmh!... kwamba ukweli ukitumia..."***

***Mchangiaji: "mchuzi wa pweza ...ee supu ya pweza eee inakuongezea libido sexual desire...sasa mkikutana wote mna nguvu ya hatari? Weka fire extinguisher"***

***Mtangazaji 1 (akijibu): "aaah anazaliwa Christiano Ronaldo hapo...(kicheko)...***

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

Kwa kitendo cha kutangaza kipindi chenye maudhui ya kuhamasisha ufanyaji wa vitendo vya ngono, **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** inatuhumiwa kukiuka Kanuni Na. 11 (c), 12(1) (a), (d), na 14 (a), (b) na (c) za Kanuni za Mawasiliano ya

Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018, ambazo zinasomeka kama ifuatavyo:

*11.-(1) A licensee shall ensure that the programme and its presentation-*
*(c) observes good taste and decency;*

*12.-(1) A content services licensees shall-*
*(a) ensure that due care is exercised in order to avoid content which may disturb or be harmful to children;*
*(d) protect children from negative influences.*

*14. Every content services licensee shall not provide content-*
*(a) unsuitable for children when large numbers of children may be expected to be part of the audience;*
*(b) which depicts or contains scenes of violence, sexually explicit conduct or offensive language intended for adult audiences during watershed period;*
*(c) which contains excessive and gross offensive language used in content transmitted during the watershed period.*

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI.

Tarehe 19 Juni, 2020, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO,** wito wa kuwasilisha utetezi wao wa maandishi pamoja na kufika mbele ya Kamati ya Maudhui kujieleza dhidi ya tuhuma zinazowakabili.

Tarehe 23 Juni, 2020, Uongozi wa **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** uliwasilisha utetezi wa maandishi uliosainiwa na **Sheba Kussaga**, Mkurugenzi wa Biashara na Maendeleo wa Kituo. Pia, tarehe 24 Juni, 2020, Uongozi huo ukiwakilishwa na **Sheba Kussaga**, Mkurugenzi wa Biashara na Maendeleo, pamoja na **Sebastian Maganga**, Mkuu wa Maudhui wa Kituo ulifika mbele ya Kamati kutoa utetezi.

## 4.0 KUSOMEWA SHITAKA NA KUSIKILIZA MAUDHUI YA CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO.

Kamati ya Maudhui iliusomea Uongozi wa **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** shitaka lao. Pia, Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** walisikiliza maudhui yaliyochapishwa na kutangazwa na **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** tarehe 04 Juni, 2020 na kisha kuualika Uongozi huo kujitetea ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni.

## 5.0 UTETEZI WA CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO

Katika maelezo yao ya maandishi**, CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** walidai kuwa lengo/nia ya kipindi chao ilikuwa ni kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutumia mazao ya baharini

kwa ajili ya kuongeza virutubisho mwilini na hiyo inatokana na minong'ono iliyopo kwenye jamii kuhusu changamoto zinazojitokeza kwa baadhi ya wanandoa.

Pia, **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** ilitoa utetezi wao wa mdomo kama ifuatavyo:

5.1 **Sebastian Maganga** alianza kwa kurudia maelezo yao ya maandishi na kisha kuendelea kueleza kuwa nia ya mjadala wao ilikuwa ni njema na waliweka kiwango cha tafsida lakini katika uwasilishwaji wa maudhui yao, walitengeneza chombezo ambalo huenda ndiyo limeleta tatizo/ukakasi kidogo. Aliendelea kudai kwamba mwishoni mwa kipindi, watangazaji walileta masihara kidogo. Alisema kuwa katika mazingira hayo wanakiri udhaifu uliojitokeza na kama mjadala ungejikita kisayansi na kutafuta majibu zaidi ya kisayansi labda wasingefikishwa mbele ya Kamati. Alimaliza kwa kukiri kuwa maudhui yao ya kufunga mjadala yanaweza kuwa yaliwakwaza wasikilizaji wengine japokuwa dhamira yao haikuwa mbaya.

5.2 **Sheba Kussaga** alianza kwa kuunga mkono maelezo ya **Sebastian Maganga** na kudai kuwa maudhui yao yalilenga kuchangia kuielimisha jamii kuhusu utafiti wa MUHAS kwa kuwa wamekuwa wakipata malalamiko mengi ya kuvunjika kwa ndoa. Aliendelea kudai kuwa kama wangeishia kwenye uthibitisho wa kisayansi isingeleta shida lakini mwishoni watangazaji walipatwa na msisimko na kuongea maudhui yanayoweza kuleta ukakasi kwa watoto waliosikiliza kipindi kile. Wakati akiulizwa maswali na Kamati, **Sheba Kussaga** alikiri kuwa kipindi chao kilirushwa katika muda usio sahihi.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

Ifuatayo ni tathmini ya Kamati baada ya kusikiliza utetezi wa **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO;**

**6.1** Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** imetenda kosa la kutangaza maudhui yenye kuhamasisha ufanyaji wa vitendo vya ngono na yanayowahusu watu wazima katika muda usio sahihi, muda ambao wasikilizaji wanaweza kuwa watoto. Hivyo, wameshindwa kumlinda mtoto dhidi ya maudhui yasiyofaa na yanayoweza kumsababishia kuiga tabia mbaya. **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** walitakiwa kutangaza maudhui yanayowahusu watu wazima katika "watershed period" ambao ni muda wa kuanzia saa sita usiku hadi saa kumi na moja alfajiri kwa mujibu wa Kanuni Na. 3 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kiektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018 kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia **Tangazo la Serikali Na. 400/2018;**

6.2 Kamati ya Maudhui imejiridhisha kuwa wasimamizi na watangazaji wa kipindi cha **Jahazi** cha **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** hawakuzingatia Weledi na Maadili ya Utangazaji wa Habari katika uwasilishaji wa maudhui yao kwa sababu ni wazi kuwa lugha mbovu

waliyoitumia katika kipindi ililenga zaidi katika kushabikia vitendo vya ngono badala ya kuelimisha jamii;

6.3 Pia, Kamati ya Maudhui imeona kuwa kipindi kilichotangazwa na **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** hakikufanyiwa maandalizi ya kutosha na hivyo badala ya kuelimisha kikawa cha kushabikia vitendo vya ngono;

6.4 Hivyo, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** imetenda makosa ya kutangaza maudhui yasiyo na staha, yenye kuhamasisha ufanyaji wa vitendo vya ngono, yasiyomlinda mtoto na katika muda usio sahihi kama ilivyotathiminiwa hapo juu na kama ambavyo wao wenyewe wamekiri, Kinyume na Kanuni Na. 11 (c), 12(1) (a), (d), na 14 (a), (b) na (c) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018.

## 7.0 USHAURI WA KAMATI KWA CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO.

Kutokana na makosa yaliyobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** kuimarisha usimamizi wa vipindi vyao ili kuepuka uvunjaji wa Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari;

Pia, **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** wanashauriwa kuhakikisha wanawapatia watangazaji wao mafunzo ya mara kwa mara ya Uandishi na Utangazaji wa Habari ili kuweza kuepuka makossa ya kizembe.

## 8.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kuutafakari kwa kina utetezi uliowasilishwa na Uongozi wa **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO**, Kamati ya Maudhui imeridhika pasi na shaka kuwa **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO** kupitia kipindi chake cha **Jahazi** wamekiuka Kanuni tajwa za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018.

Hivyo basi, Kamati ya Maudhui inatoa adhabu zifuatazo kwa **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO:**

1. Wanapewa Onyo Kali pamoja na kutahadharishwa kuwa hatua kali zaidi za kisheria zinaweza kuchukuliwa dhidi yao iwapo hawatajirekebisha na kurudia makosa kama hayo;

2. Wanatozwa faini ya **Shilingi Milioni Tano (TZS. 5,000,000.00)** tu, itakayolipwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);

Uamuzi huu umetolewa Dar es Salaam, leo tarehe **01 Julai 2020**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia siku ya kutolewa kwa uamuzi huu.

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Joseph Method Mapunda**

…………………………………………………

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WAFUATAO WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Abdul Ramadhani Ngarawa**………………………………
2. **Derek Kaitira Murusuri**………………………………
3. **Jacob Gregory Tesha**………………………………